# OFISI YA RAIS

# TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

# HALMASHAURI YA WILAYA YA NKASI

Shule Ya Sekondari Sintali

S.L.P 492

**Nkasi – Rukwa**

Simu: *0627256589/0765890142*

**Tarehe** ……………………………

**KUMB.NA.SSS/F.IJOINS/2021/VOL1**

**NDUGU** ………………………………………

**S.L.P**………………………………………………

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI SINTALI**

Ninayo furaha kukujulisha kuwa umechaguliwa kujiunga na Shule Ya Sekondari Sintali baada ya kufaulu mtihani wako wa darasa la saba. Utapokelwa katika shule hii kuanza masomo ya kidato cha kwanza mwaka *2021*. Shule itafunguliwa tarehe **11-01-2021**. Tafadhali wahi bila kukosa.

Shule hii ipo **Wilaya Ya Nkasi, Kata Ya Sintali, Kijiji Cha Nkana**. Ni shule ya kutwa na ina huduma ya malazi(hostel) ***kwa wasichana tu***.

## MAHITAHI YA SHULE

### 1. SARE ZA SHULE

**WASICHANA**

*i.* Sketi mbili za rangi nyeusi na damu ya mzee, ziwe ndefu zinazogusa viatu. *(Sketi fupi isiyogusa viatu haitaruhusiwa kuvaliwa shuleni)*

ii. Mashati mawili meupe mikono mifupi

iii. Soksi nyeupe fupi jozi mbili

iv. Viatu vyeusi vya kamba, viwe na kisigino kifupi



Scanned with CamScanner

v. Raba kwa ajili ya michezo
vi. Sweta rangi ya zambarau
vii. Tai nyeusi na damu ya mzee
viii. Kwa wanafunzi wa hostel waje na chandarua, godoro furi 3 ½ , sanduku la chuma(tranka), shuka mbili za rangi ya pinki, sahani, bakuli, kijiko na kikombe.
ix. Truck suit ya rangi ya bluu
x. Shamba dress (Gauni la rangi ya damu ya mzee – moja)

**MUHIMU**: *Wanafunzi Wa Hostel Wasije Na Nguo Za Nyumbani Maana Hazitatumika Kwa Muda Wote Wawapo Shuleni.*

**WAVULANA**

i. Suruali mbili za rangi nyeusi na damu ya mzee
ii. Mashati meupe mawili yenye mikono mifupi
iii. Soksi nyeupe fupi jozi mbili
iv. Viatu vyeusi vya kamba vyenye kisigino kifupi
v. Raba kwa ajili ya michezo
vi. Sweta rangi ya zambarau
vii. Tai yenye rangi nyeusi na damu ya mzee
viii. Truck suit ya rangi ya bluu***(hii ni muhimu sana kwani mwanafunzi haruhusiwi kuvaa nguo za nyumbani wakati wa shughuli za nje au muda wa masomo ya jioni)***

2. VIFAA VYA DARASANI

i. Daftari kubwa kumi (10) aina ya counter book
ii. Set ya vipimo vya hisabati (mathematical set)
iii. Kalamu ya risasi (penseli)
iv. Kalamu ya wino
v. Dictionary (kamusi) ya kiingereza kwa kiswahili
vi. Rula

3. MAHITAHI MENGINE

i. Ufagio
ii. Leso(*Handkerchief*)
iii. Mche mmoja (1) wa mti aina yoyote
iv. Cheti cha kuzaliwa



Scanned with CamScanner

## SHERIA ZA SHULE

1. Sare za shule zisiwe na urembo wa aina yoyote
2. Kila mwanafunzi awe na nywele fupi zinazofaa kuchana kwa urahisi. Mapambo kama vile hereni, mikufu, mapambo ya nywele, kucha ndefu, kufuga ndevu **NI MARUFUKU**
3. Kila mwanafunzi anatakiwa kutii wito wa kengele
4. Ni marufuku kupiga kelele darasani au kutoka nje ya darasa bila ruhusa
5. Ni marufuku kuzungumza lugha ya kiswahili maeneo ya shule
6. Mwanafunzi anatakiwa kusimama na kumsalimu mwalimu au mtu yoyote anayemzidi umri anapopita ndani au nje ya mazingira ya shule
7. Mwanafunzi anatakiwa kumpokea mzigo aliobeba mwalimu au mgeni yoyote ajaye shuleni
8. Mwanafunzi anatakiwa kutumia lugha ya heshima kwa walimu, wanafunzi na watu wengine pia
9. Ni marufuku kwa mwanafunzi kuwa na simu shuleni
10. Ni marufuku kutoka nje ya mipaka ya shule bila idhini kutoka kwa uongozi wa shule

## MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA SHULE

a) Uasherati na uzururaji
b) Wizi
c) Kuchezea au kuharibu bendera ya taifa
d) Kupigana, kutukana na kunyanyasana
e) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
f) Kutoroka shule
g) Kunywa pombe, kuvuta sigara/bangi au kutumia madawa ya kulevya
h) Ubaguzi wa aina yoyote
i) Kuoa au kuolewa
j) Kupata mimba au kusababisha mimba nje au ndani ya shule
k) Kutoa mimba
l) Kugoma, kuchochea au kuvuluga amani na usalama wa shule
m) Kukataa adhabu kwa makusudi
n) Kuwa na simu ya mkononi



Scanned with CamScanner

## FOMU YA KIAPO NA AHADI KWA MWANAFUNZI

Mimi ……………………………………………………………naahidi kuwa nitafuata sheria zote za shule zilizowekwa na uongozi wa shule, na kuwa nitazitii kwa wakati wote nikiwa mwanafunzi. Iwapo nitakiuka sheria hizo, hatua kali za kinidhamu zichukuliwe dhidi yangu.

**SAHIHI YA MWANAFUNZI……………………………………. TAREHE…………………….**

**SAHIHI YA MZAZI/MLEZI………………………………….. TAREHE…………………..**

**KARINU SANA SHULE YA SEKONDARI SINTALI**

**MOTTO WETU:- "ELIMU NI MAENDELEO"**

***(EDUCATION IS DEVELOPMENT)***

……………………………

**REMMY, R.E**

**MKUU WA SHULE**

THE HEADMASTER
P.O.Box - 492
NKASI
SINTALI SECONDARY SCHOOL



Scanned with CamScanner

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

MINISTRY OF EDUCATION, SCIENCE AND TECHNOLOGY

SINTALI SECONDARY SCHOOL

**TO THE MEDICAL OFFICER**

**…………………HOSPITAL**

**P.O BOX ………….**

………………………..

Please, examine the student…………………………………………, the following

1. Epilepsy
2. Vision
3. Hearing
4. Pregnancy
5. Other problems that can lead him/her not to be able for schooling or any other problem that will need him/her, stay close to hospital
   ………………………………………………………………………………………………
   ………………………………………………………………………………………………
   ………………………………………………………………………………………………
   ………………………………………………………………………………………………

I have examined the above named student and proof that he/she is fit/not fit for schooling.

**Signature……………………………… Title……………………………………………**

**Date ……………………………………**

**Official Stamp**

…………………………………

**"USIJE BILA KUKAMILISHA FOMU HII"**



Scanned with CamScanner